Teacher.co.ke

**MUHULA WA PILI 2023**
**KISWAHILI**
**KIDATO CHA KWANZA (1)**
**MUDA: SAA 2 ½**

## MWONGOZO

### Ufahamu (alama 15)

a) MASOMO/SHULE MBALIMBALI (1x1=1)

b) Shule za umma na Shule za kibinafsi (2x1= 2)

c) i) Kutembea kilomita nyingi kutafuta rasilimali muhimu kama maji, kupata chakula,
ii) Mafuriko katika msimu wa masika,
iii) Shule nyingi hazina miundombinu muhimu,
iv) Kukosa vifaa muhimu vya masomo ya kisayansi,
v) Kuzongwa na majukumu mengine nyumbani kama vile ulezi n.k(zozote 3x1=3)

d) Wa kutwa wamekosa mafuta ya taa ili kufanya udurusu lakini wa bweni wana stima – au hata jenereta endapo stima zitapotea.

Wa kutwa wanapokosa chakula, wa bweni wanakula na kusaza (2x1=2)

Teacher.co.ke

e) watakosa nafasi za kujiunga na chuo kikuu
Watakosa kazi. (2x1=2)

f) hakutaondoa werevu walionao au kuwanyima uwezo wa kutimiza **maazimio** yao (2x1=2)

g) maana ya msamiati
i) kudura; matakwa/amri/Nguvu za Mungu
ii) maji walikwishayavulia nguo; walishaamua
iii) maazimio; malengo (3x1=3)

## A. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) /t/; sighuna / hafifu
/d/; ghuna (2x1=2)

b) i) pigo la sauti katika neno (1x1=1)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

ii) a-li-m-**fyo-nza** (2x1=2)

c) i) Viungo vinavyoambatanishwa kabla au baada ya mzizi ili kuleta maana maalum. (1x2=2)

ii) Wa-ta-shon-ew-a

wa, -ta; awali

-ew, -a; tamati (2x1=2)

d) Mfano: imba, embe , enda n.k (1x1=1)

e) Lo!; kihisishi (I) yote; kiwakilishi(W)

Wanafunzi ; nomino (N)

werevu; kivumishi (V)

sana ; kielezi(E) (6 x ½= 3)

walijibu; kitenzi (T)

f) Wanafunzi waliona baraste, njia

wanafunzi waliona sawasawa (2x1=2)

g) M-WA; mtu-watu

M-MI; mtume-mitume

KI-VI; kiroboto-viroboto

Ø-MA; daktari-madaktari

Ø-Ø; shangazi-shangazi (yoyote 3x1=3)

h) Kiswahili ni lugha ya kuvutia. (taarifa)

Tafadhali tulieni. (rai/ombi)

Unataka nini hapa? (swali)

Ondokeni mara moja! (amri/agizo)

Lo! Ameiba pesa ya mwalimu. (mshangao) (3 x1 =3)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

i) Wote watundu; kundi nomino (KN)

walicheza nje kabla ya muda ufaao;kirai kihusishi ; Kundi tenzi(KT) (2x1=2)

j) Wanafunzi wa kidato cha kwanza ni wangwana sana. (2x1=2)

k) S-KN(N+V+E) + KT (T+H)

Chakula kitamu sana kilipikwa chini ya mti. (1x2=2)

l) Ugali wote uliliwa na Amina. (1x2=2)

m) Jiti hilo lilikatwa asubuhi. (1x2=2)

n) **J**e, **K**haemba na **T**afari walifunga ngo'mbe**?** (6 x ½=3)

o) Ninapenda kula na kunywa. (1x2=2)

p) shuka ; teremka kutoka juu

suka; pitisha chane za ukindu wakati wa ususi. (2x1=2)

q) Mtaka cha mvunguni sharti ainame . (1x2=2)

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) i) Kiswahili ni lugha ya mseto.

ii) Kiswahili ni lugha ya kiarabu.

iii) Kiswahili ni kibantu

iv) Chanzo cha Kiswahili ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

(4x1=4)

b).

i. Ni somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za msingi na upili
ii. Ni lugha rasmi ya pili nchini Kenya.
iii. Ni lugha ya taifa nchini Kenya.
iv. Inatumiwa katika vyombo vya habari; runinga, magazeti na redio
v. Inatumiwa katika shughuli za kidini.
vi. Inatumiwa kuchapisha vitabu
vii. Inatumiwa na vyombo vya usalama na sheria
viii. Inatumiwa katika shughuli za sanaa,maonyesho na muziki.
ix. Inatumiwa kuendeleza biashara
x. Kumezinduliwa vyombo na vyama vya kukuza na kueneza Kiswahili kama vile CHAKITA.
xi. Ujenzi na upanuzi wa msamiati wa Kiswahili.
xii. Matumizi ya Kiswahili mtandaoni na katika tarakilishi. (6x1=6)

**FASIHI SIMULIZI(Alama 15)**

a) Hadithi (1x1=1)

b) i) Hapo zamani za kale/za kongamawe…
ii) Hadithi! Hadithi! Hadithi njoo…

iii) Kaondokea chenjangaa, kajenga nyumba kakaa, mwanangu mwanasiti, kijino kama chikichi, cha kujengea kikuta, na vilango vya kupita…

iv) Hapo jadi na jadudi… (2x1=2)

a) i) mwenye tamaa
ii) mwongo
iii) mwenye hasira
(aeleze) (2x2=4)

d) Aliogopa kumkabili nyanya-mtu baada ya kumdanganya (1x2=2)

e)

**i.** Awe jasiri; asiwe mwoga ili kuweza kuzungumza hadharani.
**ii.** Asiwe na haya ili kuweza kuzungumzia mambo ya aibu inapobidi.
**iii.** Awe na uelewa wa mazingira na masuala ibuka katika jamii ili kuweza kuwasilisha dhana zisizopatikana katika mazingira yake k.m. kutumia rais kuelezea dhana ya mfalme.
**iv.** Awe na ufahamu mpana wa lugha ili aweze kuitumia kwa uhodari na kuwasilisha kwa wepesi.
**v.** Awe mchangamfu na mcheshi ili kunasa makini ya hadhira na kuzuia isikinai.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

vi. Awe na ufahamu mpana wa utamaduni husika ili kuzuia kutumia maneno na ishara zinazoweza kuwaudhi au kupingana na imani za hadhira.
vii. Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira k.v. kuimba, maswali ya balagha ili isikinai, n.k.
viii. Aweze kujua, matarajio, kiwango cha elimu na tajriba ya hadhira ili kuweza kubadilisha kwa kiwango kinachofaa.
ix. Awe na uwezo wa kuingiliana vizuri na hadhira ili aivutie.
x. Awe na kumbukumbu nzuri ili usimulizi wake utiririke vizuri.
xi. Awe na sauti nzuri ili avutie na asikike vyema
xii. Awe na ujuzi wa kutumia viziada lugha kv ishara za uso, mwili na miondoko kulingana na hali anayoigiza.
xiii. Aweze kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti anazoigiza k.v. huzuni
xiv. Awe na uwezo wa ufaraguzi/ kubadilisha utambaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake na kutoa mifano inayofahamika kutoka katika mazingira ya hadhira. (za kwanza 8x1=8)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes